# KICHAKA CHA FEDHA CHENYE ASILI YA 'CHUMA ULETE'

02 Julai, 2020



Najua si mimi pekee ninayeisaka Shilingi kwenye mahandaki na nisipate chochote. Nilitamani siku moja nijue mahali fedha zilikopelekwa angalau nijiridhishe kuwa, zilikuwepo lakini zimetumika kufanyia jambo fulani. Pia lisingefanywa jambo hilo, mwenyewe nisingeweza au ningeweza kwa shida nyingi.

Sikugundua kichaka hiki moja kwa moja bali nilikuwa ninataka kupima malalamiko ya wananchi kuhusu hali ya maisha kuwa 'vyuma vimekaza.' Mimi sio Mchumi hivyo sikufua dafu.

Nilijaribu kutumia fani yangu ya ualimu kulinganisha malalamiko ya mishahara na kazi zinazofanywa na waajiriwa hao na matokeo ya kazi zao. Mbaya, niliangalia upande wa elimu na shule.

Zig zag niliyokutana nayo ilinipa ugumu kupata majibu. Yaani kupima matokeo ya utendajikazi ukilinganisha na uwekezaji uliofanyika.

ELIMU; Mitaala, vitabu, mitihani, ukaguzi na shughuli za kielimu zinasimamiwa na Wizara ya elimu. Walimu na utumishi vipo chini ya TAMISEMI. Elimu za walimu na taasisi za elimu ya juu zipo Wizara ya Elimu sayansi na teknolojia. Fedha zipo Hazina chini ya Wizara ya fedha (kazi yao ni kufanya malipo) wakati ajira zinaandaliwa na Wizara ya ajira katika ofisi ya Waziri Mkuu. Hapa napo sikupata jibu! Niliishia kushangaa zigzag hii aliiweka nani na lengo lake lilikuwa ni nini? Pongezi nyingi ziwafikie Wizara ya Afya sababu wao wangelikuwa na zigzag hii nahisi Corona ingetumaliza sote.

Nilimkumbuka mwalimu wangu wa physics aliposema; sio lazima upande kwenye gari na kuanza kusoma 'speed meter' ili kugundua mwendo wa gari au

kumuuliza dereva alitembeza gari kwa ‘speed’ gani. Bali utajua endapo utakuwa na ‘data’ zenye kueleza umbali na muda uliotumika.

Hapa ndipo nilipokutana na KICHAKA cha fedha. Watu wengi wanajua wanafunzi wanaosoma shule za serikali wanapata elimu bure hivyo ni bure kabisa.

Wengine wanakufuru kwa kuziita shule hizo majina ya dharau. Wakiamini hata kama serikali ikiacha kulipia gharama za elimu, wao watamudu kulipia gharama zote. Sidhani kama balaa hilo likianzishwa kuna mtoto wa mkulima anayetegemea mvua inyeshe ndipo apate ridhiki akatoboa kufanikisha watoto wake kupata elimu. Ada halali za shule za serikali sio Tsh. 40,000 wala 100,000 ni zaidi ya hiyo.

Nikiwa ninaandika kitabu changu mwaka 2016 niliweka wazi KICHAKA hiki na ilikuwa hivi;
Ili shule iendelee inahitaji kuwekeza mtaji mkubwa kama majengo, rasilimali watu na vitendea kazi pamoja na miundombinu mingine.

Nilichukua mshahara peke yake anaolipwa mwalimu aliyeanza kazi na kufanya kazi hiyo kati ya miaka 3 hadi saba. Tsh. 940,000/= Nilizidisha mara 12 ili

kupata mshahara wa mwaka mmoja kwa mwalimu 1 na kupata Tsh 11,280,000/= Shule ya mfano ilikuwa na walimu 23 hivyo nilizidisha 11,280,000×23= 259,440,000Tsh. Ingawa walikuwepo walimu waliopokea mshahara mkubwa zaidi ya 1m mfano wenye daraja F. Na wengine pungufu. Hii ilikuwa mishahara ya 2016 kwa sasa imeongezeka.

Ili kujua ufanisi wa kazi, nilichukua malipo ya mshahara wa walimu kwa mwaka kugawanya kwa idadi ya wanafunzi. Shule ilikuwa na wanafunzi 187. Hivyo 259,440,000 ÷187=1,387,379.68/= Hivyo kila mwanafunzi alilipiwa na serikali Tsh. 1,387,379.68 kwa mwaka kuwalipa mshahara walimu pekee bila elimu bure, wala chakula, wala ukarabati, na stahiki zingine za mwalimu na gharama za uendeshaji wa shule.

Cha ajabu matokeo ya mitihani mwishoni mwa mwaka waliofaulu kwenda kidato cha tano ni wanafunzi kati ya 0 hadi 5.

Hivi hii SIO CHUMA ULETE? Unalipa mafundi 200M kujenga nyumba halafu mwisho wa mradi

unakuta hata tofali moja halijajengwa, hivi hiyo ni haki?

Ninajua kuna watu wanasubiri kampeni zianze, wakumbushe Tshilingi milioni hamsini (50) zao kwa kila kijiji. Sasa fikiria ndani ya miaka minne kijijini kwenu au mtaani kwenu walihitimu wanafunzi wangapi katika shule za msingi na sekondari za serikali? Katika kila shule moja kulikuwa na wanafunzi wangapi? Na ikiwa kila mmoja wao, serikali ilimlipia zaidi ya Tsh. Milioni moja (1) kwa mwaka, jumla ni Tshilingi ngapi?

Ni miaka minne tu tangu niandike kitabu hicho, mwaka huu kuna kiongozi aliweka pingamizi la fedha za elimu. Unafikiri OFA hii inaweza kuendelea milele? Ikiwa wanafunzi waliolipiwa na wazazi wao na kufaulu wote shule mzima wakiwa na weledi mkubwa na maarifa yaliyotukuka watakuja kuendelea kulipa gharama hizi, ikiwa wao walisomeshwa na jasho la wazazi wao na kulelewa na patron na matron wakiwa watoto wengine wanakula *'bata'* na familia?

Watu hao sasahivi wapo vyuo vikuu tayari. Siku si nyingi watakuwa wamechukua soko lote la ajira.

Wanaroho ya upweke sababu ya malezi waliyoyapata yaliyokosa upendo wa familia.

***FEDHA zenu zipo kwa watoto unaowaona wamevaa sare lakini hawapo 'serious' na masomo wakiamini wanapata, "vya bure" na bure haina thamani. Wazazi wao wapo kimya, sababu wanajua kila kitu ni bure tena bure kabisa na matokeo ni bure!***

Wanafunzi wote wangezingatia masomo wangeweza kufika kwenye hatua ya uzalishajimali hivyo taifa lisingelikuwa na idadi kubwa ya wategemezi.